## 10.0 UKAGUZI WA BIDHAA HAPA NCHINI

Shehena za bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambazo hazijakaguliwa kabla ya kusafirishwa na kupewa cheti cha ubora (CoC), zitakaguliwa na kupimwa na TBS zitakapofika nchini, baada ya mwagizaji kulipa faini.

Pia kuna vigezo vilivyowekwa ili bidhaa zinazotakiwa kupitia mfumo huu kuweza kugakuliwa hapa nchini bila kutozwa faini. Orodha ya vigezo hivyo inapatikana katika tovuti ya TBS, **www.tbs.go.tz/Compliance and Enforcement/Imports and Export Control/Pre-shipment Verification of Conformity.**

Baada ya bidhaa husika kupimwa na kuonekana kukidhi matakwa ya kiwango, cheti cha kuthibitisha ubora wa bidhaa hiyo hutolewa kwa shehena husika na kupelekwa kwa Kamishna wa Forodha ambapo hutumika katika kutolea mzigo.

Bidhaa kutoka nje ya nchi ambayo iko chini ya kiwango hairuhusiwi kuingia katika soko la Tanzania. Hivyo, hairuhusiwi kutoka bandarini au mpakani hadi majibu ya maabara yatakapokuwa yametoka na kuonyesha kuwa bidhaa imekidhi matakwa ya viwango husika.

Aidha, shehena yenye CoC inaweza kuchukuliwa sampuli na kupimwa/ kukaguliwa kwa ajili ya kujiridhisha kuwa taratibu zilifuatwa kama inavyotakiwa. Katika hili, TBS huhitaji ushirikiano wa mwagizaji. Shehena hii itahitaji kutolewa kwa masharti ya kutouzwa hadi ripoti ya upimaji/ ukaguzi itakapotolewa baada ya siku nne.

**Utaratibu wa ukaguzi ni kama ifuatavyo:**

- Maombi ya ukaguzi
- Ukaguzi wa shehena na kuchukua sampuli
- Upimaji wa sampuli katika maabara ya TBS
- Utoaji cheti

**Gharama ni kama ifuatavyo:-**

| Na | MAELEZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|
| | Ada ya ukaguzi | 100,000 |
| | Ada ya upimaji | Hutofautiana kulingana na bidhaa husika |
| | Ada ya udhibiti wa shehena | 6/Kg kwa mizigo mingine au 2.5/Kg kwa sukari pekee |

Muagizaji wa mzigo atalazimika kurudisha bidhaa itakayogundulika kutokidhi matakwa ya viwango katika nchi alikotoa bidhaa hiyo au kulipia gharama za uteketezaji wa bidhaa husika kama uteketezaji wake hauna athari kwa mazingira.

## 11.0 UKAGUZI WA MAGARI YALIYOTUMIKA KABLA YA KUSAFIRISHWA

Ili nchi yetu isigeuzwe kuwa jalala la magari yaliyotumika na yasiyofaa kwa matumizi ya barabarani, TBS ilianzisha utaratibu wa kukagua na kupima magari hayo kabla hayajasafirishwa kuja nchini.

Wakala anaekagua magari yaliyotumika kwa niaba ya TBS ni kama ifuatavyo:-

| SN | WAKALA | NCHI | GHARAMA (USD) |
|---|---|---|---|
| 1 | East Africa Automotive Service Company Limited (EAA) | Japan | 150 |
| Mawakala wanapatikana kwa zabuni, hivyo wanabadilika kipindi cha mkataba kikiisha. | | | |

Waagizaji wote wanatakiwa kukagua na kupima magari yao katika Nchi gari linakotoka katika kampuni hiyo kabla ya kuyasafirisha kuja nchini. Gari lililotumika litakalofika nchini bila ya kuwa na cheti cha ukaguzi litatozwa faini ya 30% ya gharama ya ununuzi na usafirishaji (C&F) na pia muagizaji atalipia gharama za ukaguzi hapa nchini.

**Kwa maelezo zaidi,wasiliana nasi kwa anwani zifuatazo:**


**MKURUGENZI MKUU**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
S.L.P. 9524, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2450298 / 2450206/2451763-6
Hotline: +0800 110 827/ Nukushi: + 255 22 2450959
Baruapepe: info@tbs.go.tz/ Tovuti: www.tbs.go.tz
Malalamiko: malalamiko@tbs.go.tz

**OFISI ZA KANDA:**
**NYANDA ZA JUU KUSINI**
(Iringa, Mbeya, Njombe and Songwe)
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S.L.P. 1674 Mbeya, Tanzania
Simu: 025 2502848 / Nukushi: 025 2502848

**KANDA YA ZIWA**
(Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu and Shiyanga)
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S.L.P. 1814 Mwanza, Tanzania
Simu: 028 2505044 / Nukushi: 028 2505044

**KANDA YA KASKAZINI**
(Arusha, Kilimanjaro, Manyara and Tanga)
Ngorongoro Tourist Center, Ghorofa ya 6
S.L.P. 2399 Arusha, Tanzania
Simu: 027 2520143 / Nukushi: 027 2520143

**KANDA YA KATI**
(Dodoma, Singida and Tabora)
Kambarage Tower, Ghorofa ya 6
S.L.P 2956, Dodoma, Tanzania
Simu: 026 2320310 / Nukushi: 026 2320310

**KANDA YA KUSINI**
(Lindi, Mtwara and Ruvuma)
Jengo la PSSSF, Sokoine House, Ghorofa ya 3
S.L.P 1396 Mtwara,Tanzania
Simu: 023 2334477 / Nukushi: 023 2334477

**KANDA YA MAGHARIBI**
(Katavi, Kigoma and Rukwa)
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S.L.P 1276 Kigoma,Tanzania
Simu: 028 2804023 / Nukushi: 028 2804023

**KANDA YA MASHARIKI**
(Dar es Salaam, Morogoro na Pwani)
Jengo la PSSSF (Commercial Complex) Ghorofa ya 4
S.L.P 9425, Dar es Salaam

TBS_Tanzania   tbs_viwango   TBS Viwango TV


# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)



# Ukaguzi wa Bidhaa zinazotoka Nje

## 1.0 UTANGULIZI

Kwa kuzingatia kifungu cha 36 (1) and 3(f) cha Sheria ya Viwango Na.2 ya mwaka 2009, Serikali ilipitisha Kanuni za Usajili wa bidhaa na Udhibiti wa Shehena – *The Standards (Imports Registration and Batch Certification) Regulations, 2021* kupitia Notisi ya Serikali Na. 681 ya Septemba 24, 2021.

Kanuni hizo zililipa TBS mamlaka ya kusajili bidhaa za chakula na Vipodozi na kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini kabla ya kusambazwa katika soko la ndani kwa nia ya kulinda nchi yetu isiwe jalala la bidhaa duni.

## 2.0 MPANGO WA UKAGUZI WA MIZIGO KABLA YA KUSAFIRISHWA KUJA TANZANIA (PVOC)

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linatekeleza mpango wa kukagua mizigo kabla ya kusafirishwa kuja nchini yaani "Pre-shipment Verification of Conformity to Standards, (PVoC)" ili kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinazoingizwa nchini zinakidhi matakwa ya viwango, kama ilivyoelekezwa katika kifungu 4(1) (s) cha Sheria ya Viwango namba 2 ya mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Sheria ya Fedha ya mwaka 2019.

Bidhaa zote zinazoingizwa nchini kama zilizoorodheshwa kupitia Mpango huu, zitahitajika kukaguliwa na kupata cheti cha uthibitisho wa kukidhi viwango, yaani "Certificate of Conformity, CoC" baada ya kukidhi matakwa ya Viwango husika.

## 3.0 MALENGO YA UKAGUZI WA MIZIGO KABLA YA KUSAFIRISHWA

- Kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinakidhi matakwa ya viwango husika kabla ya kusafirishwa kuja nchini;
- Kulinda jamii kutokana na bidhaa hafifu ambazo zinahatarisha afya, usalama na mazingira;
- Kulinda viwanda vya ndani kutokana na ushindani usio wa haki kutoka katika bidhaa zilizoagizwa na kuingizwa nchini bila ya kukidhi viwango vya ubora;
- Kuongeza ufanisi ili kwenda sanjari na maboresho ya TRA na TPA katika kuhakikisha shehena zinaondoshwa kwa haraka mara zinapofika bandarini na hivyo kurahisisha mazingira ya ufanyaji biashara;
- Kuepusha hasara kwa mwagizaji wa bidhaa anapoingiza bidhaa hafifu na kulazimika kurudisha alikoiagiza au kuharibu;
- Kuepusha kuharibu mazingira kwa kuharibu bidhaa hapa nchini;
- Kuweka uwiano katika mfumo wa ukaguzi wa bidhaa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## 4.0 MAMBO YA KUZINGATIA

- Bidhaa zinazoagizwa na kusafirishwa kuja Tanzania zilizopo kwenye orodha ya bidhaa zinazotakiwa kukaguliwa kabla ya kusafirishwa kuja nchini ni lazima zikaguliwe na kupewa cheti cha ubora (CoC) kama uthibitisho wa kukidhi viwango.
- Cheti cha uthibitisho wa kukidhi viwango (CoC) ni lazima ili kuruhusiwa kuondosha mzigo wako bandarini, uwanja wa ndege au mpakani mwa Tanzania na nchi nyingine.
- Bidhaa ambazo hazipaswi kukaguliwa kabla ya kusafirishwa zitakaguliwa na Shirika la Viwango Tanzania mara baada ya kufika nchini.
- Muagizaji atabeba dhamana ya mzigo wowote utakaoingizwa nchini bila cheti cha uthibitisho wa kukidhi viwango (CoC).
- Ni jukumu la mwagizaji, msambazaji/muuzaji au mzalishaji wa bidhaa kuhakikisha bidhaa zake zinakidhi viwango.

## 5.0 UTARATIBU WA KUFUATA ILI KUKAGUA MIZIGO

Ili kupata cheti cha ubora msambazaji/mnunuzi ni lazima:

- Achague wakala anaetambulika kisheria na Shirika la Viwango ili akague shehena yake. Mawasiliano yafanyike kupitia Anuani za mawakala zinapatikana kwenye tovuti yetu, www.tbs.go.tz.
- Awasilishe fomu ya kuomba ukaguzi iliyokwishajazwa ikiambatishwa na ankara kifani (proforma invoice.
- Awasilishe ripoti ya maabara, vyeti vya umahiri vya maabara au vyeti vya mfumo wa udhibiti ubora. Ripoti hiyo lazima iendane na shehena.
- Wakala wa ukaguzi atahakiki njia na viwango vitakavyotumika kukagua
- Wakala wa ukaguzi anaweza kuchukua sampuli kwa uchunguzi wa kimaabara.
- Ukaguzi utafanyika endapo tu utaratibu ulioainishwa hapo juu utafuatwa na malipo yote ya ukaguzi kufanyika.

## 6.0 MAABARA ZINAZOKUBALIKA AU ZILIZOIDHINISHWA

- Maabara za wakala wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS);
- Maabara zilizoidhinishwa kutokana na umahiri au kutekeleza kiwango cha kimataifa cha ISO/IEC 17025;
- Maabara ya mwenye kiwanda chini ya usimamizi wa wakala wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

## 7.0 NJIA ZA KUKAGUA MZIGO

- **NJIA A**: Inatumika kwa aina yoyote ya mzigo na mfanyabiashara yeyote, msambazaji au mzalishaji ambaye hajasajiliwa.
- **NJIA B:** Inashauriwa kwa wale wanaotuma au kuagiza mizigo ya aina moja mara kwa mara. Njia hii inahitaji usajili wa bidhaa husika.
- **NJIA C:** Hii ni kwa ajili ya wazalishaji wa bidhaa zinazokidhi viwango ambao mifumo yao ya udhibiti ubora imehakikiwa/ imesajiliwa na wakala wa Shirika la Viwango Tanzania.

## 8.0 UTARATIBU WA MALIPO

| NJIA | Gharama ya kukagua mzigo % | Gharama ya chini kupokelewa | Gharama ya juu kupokelewa |
|---|---|---|---|
| A | 0.50 | 250 | 5,000 |
| B | 0.450 | 250 | 5,000 |
| C | 0.250 | 250 | 5,000 |

Malipo yaliyotajwa hapo juu hayahusishi:

- Gharama za vipimo vya maabara. Hivi vitagharamiwa kwa kutegemea aina ya vipimo vya bidhaa husika..
- Gharama za usajili wa bidhaa.
- Gharama za utoaji leseni kwa viwanda.

## 9.0 ADHABU ZA KUTOZINGATIA UKAGUZI CHINI YA MFUMO WA PVoC

Kuanzia Agosti 1, 2012, shehena zote zisizo na cheti cha uthibitisho wa kukidhi viwango (CoC) zitatozwa faini ya asilimia kumi na tano (15%) ya thamani ya mzigo, usafirishaji na bima (CIF), kisha kukaguliwa kwa utaratibu wa ukaguzi wa bidhaa zinapoingia Nchini, yaani *Destination Inspection(DI)*. Shehena zisizokidhi matakwa ya viwango zitarejeshwa katika nchi zilikotoka au kuharibiwa kwa gharama ya mwagizaji.

Ili kuepuka kadhia hii, waagizaji wote wa bidhaa wanaaswa kuhakikisha kuwa shehena zao zinakaguliwa na zinathibitishwa ubora na mawakala wa ukaguzi wa Shirika la ViwangoTBS ambao wana ofisi kote duniani.

Maelezo zaidi kuhusiana na mawakala wa TBS pamoja na ofisi zao duniani kote yanapatikana katika tovuti yetu, **www.tbs.go.tz**.